

# JINSI YA KUTOA TAARIFA YA UBAGUZI WA RANGI NA UBAGUZI KATIKA SHULE YA MTOTO WAKO



Swahili

**Mtoto wako anastahili kuheshimiwa, kuthaminiwa na kutendewa usawa katika jamii za shule.**

**Ubaguzi au unyanyasaji unaohusiana na dini au rangi haukulabili.**

Ikiwa wewe ni mzazi au mlezi wa mtoto ambaye amepitia uzoefu au kuona ubaguzi au unyanyasaji wa kidini au wa rangi kwenye shule yake, tunakuhimiza kutoa taarifa hiyo.

Wafanyakazi wa shule wanaweza kuhakikisha hatua zinazofaa na usaidizi unatolewa.

Unaruhusiwa au unaweza kutoa malalamiko rasmi kuhusu tukio hili kwenye shule au ofisi ya mkoa.

Kwa habari zaidi, tazama:

[Toa malalamiko au suala kuhusu shule yako \(education.vic.gov.au\)](http://Toa malalamiko au suala kuhusu shule yako (education.vic.gov.au))

## TOA TAARIFA YA TUKIO KWA SIMU YA KURIPOTI UBAGUZI WA RANGI (REPORT RACISM HOTLINE)

### Report Racism Hotline

1800 722 476

[report.racism@education.vic.gov.au](mailto:report.racism@education.vic.gov.au)

Simu hii inapatikana kutoka saa 3 asubuhi hadi saa 11 jioni (9am -5pm), Jumatatu hadi Ijumaa, isipokuwa sikukuu za umma.

Kama hujisikii vizuri kutoa taarifa ya tukio kwenye shule ya mtoto wako, au kama hujafurahishwa na majibu ya shule, unaweza kuwasiliana na Report Racism Hotline ya Idara.

Wakati unapopiga simu kwa simu hiyo, utaweza:

- kujadiliana kuhusu kutoa malalamiko
- kufikiria chaguzi zinazopatikana na unachoweza kufanya baadaye
- kupata usaidizi kuwasiliana na maafisa wa mkoa na huduma za msaada.

## PATA USHAURI NASAHA NA USAIDIZI WA SIMU KUPITIA PARENTLINE

### Parentline

13 22 89

[www.parentline.vic.gov.au](http://www.parentline.vic.gov.au)

Parentline inapatikana kutoka saa 2 asubuhi (8am) hadi saa 6 usiku, siku saba kwa wiki, ikiwa ni pamoja na sikukuu za umma.

Unaweza pia kutaka kupigia simu watu wa Parentline ili kupata ushauri nasaha na usaidizi kutoka kwa mshauri aliyehitimu ambaye anajitegemea kwa kutohusiana na Idara.

Parentline ni huduma ya simu ya ushauri nasaha wa siri na bila kujulikana kwa wazazi na walezi wa watoto wachanga hadi wa umri wa miaka 18. Washauri wanapatikana ili kuzungumza kuhusu masuala mengi ya uzazi, ikiwa ni pamoja na ubaguzi au unyanyasaji shulenii.

### HABARI MUHIMU

Kwa habari zaidi juu ya kutoa taarifa ya ubaguzi au unyanyasaji wa kidini au wa rangi katika shule tazama:

[Kutoa taarifa ya ubaguzi wa rangi au wa kidini katika shule \(education.vic.gov.au\)](http://Kutoa taarifa ya ubaguzi wa rangi au wa kidini katika shule (education.vic.gov.au))

Kwa habari na rasilimali zaidi kuhusu kukabiliana na uonevu, ikiwa ni pamoja na uonevu wa rangi, tazama:

[Kusimamisha Uonevu \(education.vic.gov.au\)](http://Kusimamisha Uonevu (education.vic.gov.au))



### Huduma ya Kitaifa ya Utafsiri na Ukalimani (TIS)

Wazazi au walezi ambao wanahitaji huduma za ukalimani wanaweza kuwasiliana na Idara au Parentline kwa kupigia simu kwa Huduma ya Kitaifa ya Utafsiri na Ukalimani (TIS) kwa 13 14 50.